

Kufuatilia/kuthibiti

T- Kipimo Cha Wingi Wa chembechenbe T (Kipimo cha CD4)

Chembechembe T ni nini?

- Chembechembe T ni mojawapo ya chembechembe zilizo kwenye mfumo wa kupigana na magonjwa mwilini. Mfumo wa kupigana na magonjwa husaidia mwili wako kupigana na magonjwa. Bila mfumo huu, unaweza kupatwa na magonjwa kwa urahisi sana kutoka kwenye vijidudu vya magonjwa vinavyokuzunguka kama vile vijimea (bacteria) na fangai (fungi). Chembechembe T pia hitwa chembechembe za CD4.

Chembechembe za T4 (CD4) ni nini?

- Chembechembe za T4 in sehemu ya chembechembe T mwilini wako. Husaidia pia katika kuhimarisha mfumo wako wa kupigana na magonjwa na kufanya uwe na afya njema.

Kipimo Cha Wingi Wa chembechenbe T4 (CD4) ni nini?

- Kipimo Cha Wingi Wa chembechenbe T4 (CD4) ni kipimo cha damu kinachopima namba za chembechembe za T4 (CD4) kwenye damu yako. Kipimo hiki hueleza jinsi ghani mfumo wako wa kupigana na magonjwa una afya njema na vile vile kwa kiwango gani maambukizi ya vijidudu vya ukimwi

Canadian AIDS Treatment Information Exchange
Réseau canadien d'info-traitements sida
www.catie.ca

AFRICANS IN PARTNERSHIP AGAINST AIDS
www.apaa.ca

Maamuzi juu ya matibabu ya aina mbalimbali yanahitajika kufanywa kwa kushauriana na mtaalamu aliyehitimu kwenye mambo ya afya na mwenye ujuzi juu ya magonjwa yanayoendana na maambukizi ya vijidudu vya ukimwi na matibabu atakayoamuliwa kutumiwa.

yameharibu mfumo wako wa kupigana na magonjwa. Jinsi ugonjwa huu unavyoendelea, kipimo chako cha T4 (CD4) hushuka chini.

- Kwa kawaida, mtu mwenye afya njema huwa na kiwango cha chembechembe za T4 (CD4) zaidi ya 500 katika kila micorlitre (lita 0.001) za damu. Hata hivyo, kipimo chako cha chembechembe za T4 (CD4) huweza kuwa tofauti upimapo siku moja nzima, na huweza badilika kutokana na sababu mbalimbali kama vile maambukizi ya magonjwa uliyonayo kwa kipindi hicho, jinsi ghani una uzito wa mambo akilini mwako, dawa za kinga za magonjwa ulizopata karibuni n.k. Kwa matinki hiyo, unahitajika kufanya kipimo hiki cha chembechembe za T4 (CD4) mara kadhaa kwa muda mrefu kidogo kuweza pata picha kamili na ya uhakika juu ya afya ya mfumo wako wa kupigana na magonjwa.
- Kipimo hiki cha chembechembe za T4 (CD4) husomeka kwa asilimia. Kwa kawaida mtu mwenye mfumo wa kupigana na magonjwa wenye afya njema huwa na asilimia thelathini (30%) ya chembechembe za T4 (CD4).

Kuna uhusiano ghani kati ya maambukizi ya vijidudu vya ukimwi na chembechembe za T4 (CD4)?

- Vijidudu vya maambukizi ya ukimwi ni vijimea vinavyoaminika kusababisha ukimwi. Vijidudu hivi vinapoingia mwilini mwako, ni lazima viingie kwenye chembechembe yeyote ya mwili kuweza ishi na kuzaliana. Chembechembe kuu ambayo vijidudu vya maambukizi ya ukimwi hupendelea kushambulia ni chembechembe za T4 (CD4).
- Vijidudu hivi vya maambukizi ya ukimwi vinapoingia kwenye chembechembe za T4 (CD4) na kuzaliana, chembechembe zako za T4 (CD4) zitakufa.
- Jinsi ujazo wa vijidudu vya maambukizi ya ukimwi mwilini mwako unavyozidi ongezeka, kipimo chako cha chembechembe za T4 (CD4) kitapungua.
- Jinsi kipimo chako cha chembechembe za T4 (CD4) kinavyozidi kupungua, mwili wako utakuwa na nguvu kidogo za kupigana na maambukizi. Hivyo utakuwa kwenye hatari kubwa ya kuwa mgonjwa kila mara.

Nifanyeje kuweza ongeza kipimo changu cha chembechembe za T4 (CD4)?

- Dawa za kupigana na vijidudu vya maambukizi ya ukimwi na matibabu mengine ya maambukizi haya zinaweza kukusaidia kupunguza wingi wa maambukizi ya vijidudu vya ukimwi na kukuongezea kipimo chako cha chembechembe za T4 (CD4). Kula vizuri, kupunzika kwa kutosha na kujaribu kupunguza mawazo na uzito wa mambo akilini mwako pia kunaweza kukusaidia kuwa na afya njema.

Nianze lini kutumia dawa za kupigana na vijidudu vya maambukizi ya ukimwi?

- Kipimo chako cha chembechembe za T4 (CD4) kinapokuwa kati ya chembechembe 350 na 200, itakubidi kuanza kutumia dawa za kupigana na maambukizi ya vijidudu vya ukimwi.
- Kipimo chako cha chembechembe za T4 (CD4) kinapokuwa chini ya 200 au asilimia ishirini (20%), uwezekano wa kukumbwa na maambukizi na magonjwa mengine utaongezeka. Kama utakuwa hujaanza matibabu hadi kipindi hiki, ni muhimu kutafakari kuanza na mapema.

Kuna tofauti ghani kati ya kipimo cha chembechembe za T4 (CD4) na ujazo wa vijidudu vya maambukizi mwilini?

- Kipimo cha chembechembe za T4 (CD4) na ujazo wa vijidudu vya maambukizi mwilini ni vipimo vya damu vinavyoweza kukupa maelezo juu ya afya yako na jinsi ghani vijidudu vya maambukizi ya ukimwi vimesababisha madhara mwilini mwako, ingawa vyote hueleza mambo tofauti.
- Kipimo cha chembechembe za T4 (CD4) hukueleza juu ya afya ya mfumo wako wa kupigana na magonjwa mwili. Hukueleza kwa kiwango ghani vijidudu vya maambukizi ya ukimwi vimeharibu mfumo wako wa kupigana na magonjwa. Pia huweza kukuashiria juu ya uwezekano wa kupatwa na magonjwa mengine.
- Ujazo wa vijidudu vya maambukizi mwilini hukueleza jinsi ghani vijidudu vya maambukizi ya ukimwi mwilini mwako vilivyosambaa. Hukueleza kwa kasi ghani vijidudu hivi vinazaliana. Vile vile huweza kukueleza kama dawa

unazotumia kupigana na mambukizi ya vijidudu vya ukimwi zinafanya kazi vizuri au la.

Shirika la kubadilishana maelezo juu matibabu ya ukimwi Kanada (The Canadian AIDS Treatment Information Exchange – CATIE) na Shirikisho la waafrika katika kupigana na ukimwi (Africans in Partnership Against AIDS - APAA) kwa nia nzuri kabisa wanatoa maelezo kwa watu wanaoishi na maambukizi ya vijidudu vya ukimwi/Ukimwi ambao wangependa kutawala afya zao wenyewe kwa kushirikiana na wataalamu wa afya wanaowapatia matibabu. Hata hivyo, maelezo haya yanayochapishwa au kutolewa na CATIE au APAA hayawezi kuchukuliwa kama ushauri wa kiafya. Hatushauri au kusisitiza juu ya tiba moja juu ya nyingine. Hivyo tunawashauri watumiaji ya maelezo yetu kupitia maelezo ya matibabu mengine yanayotolewa na vyanzo mbalimbali kwa upeo mkubwa iwezekanavyo. Tunawashauri watumiaji wa maelezo haya na kusisitiza kuwa ni muhimu kushauriana na wataalamu ya afya na tiba waliohitimu mafunzo yao kabla ya kuamua, kutumia au kuanza jambo lolote juu ya matibabu.

Vile vile, hatuthibitishi au kudhamini ukweli au ufarisi na ujuzi wa maelezo yanayochapishwa au kupatikana kutoka CATIE au APAA. Watumiaji wanaotumia au kutegemea maelezo haya wanafanya hivyo kwa kuthubutu wenyewe na matokeo yake yakiwa mabaya yatakuwa juu yao. Si CATIE wala APAA, au Wizara ya Afya Kanada, au wafanyakazi wao, wakurugenzi, maafisa au watu wanaojitolea wataweza kuhusishwa na uharibifu wa aina yeyote unaoweza kutokea kwa kutumia vizuri au vibaya maelezo haya. Mawazo na maelezo yaliyotolewa hapa au kwenye nakala yeyote au ilani/tangazo lolote.

Copyright: This Fact Sheet is made available through a collaboration between Africans in Partnership Against AIDS (APAA), Asian Community AIDS Services (ACAS) and the Canadian AIDS Treatment Information Exchange (CATIE). Original content developed by ACAS, 2001. Translation into Swahili and Hausa by APAA, 2004.

This information is also available in Chinese, Tagalog and Vietnamese

Funding has been provided by Health Canada, under the Canadian Strategy on HIV/AIDS

Supported by an unrestricted educational grant from GlaxoSmithKline in partnership with Shire BioChem

ACAS Asian Community AIDS Services
www.acas.org

Canadian Strategy on HIV/AIDS

gsk GlaxoSmithKline

Shire Shire BioChem